


NATIONAL RECONSTRUCTION ALLIANCE

N.R.A

KATIBA YA CHAMA



Toleo la 1-2017

SOMO LA KWANZA

IJUE NATIONAL RECONSTRUCTION ALLIANCE

(N.R.A)

UTANGULIZI.

Kwa mujibu wa sheria Na.5 ya mwaka 1992,N.R.A ni chama cha kisiasa,chenye usajili wa kudumu, kilichopata usajili wake tarehe 8/2/1993 na kupata namba ya Usjili No.00009.

MAUDHUI YA ALAMA ZA CHAMA.

I. BENDERA.

Bendera ya N.R.A ina rangi tatu.**Nyekundu,Nyeupe na Nyeusi** na alama nyingine mbili zinazoonekana katika Bendera ,Alama hizo ni **Ufagio** na **Jua linalochomoza**.

II. TAFSIRI YA RANGI ZA BENDERA.

(a) NYEKUNDU.

Hii maana yake ni ishara ya kumbukumbu ya wale wote waliokufa,waliomwaga damu yao kwa ajili ya ukombozi wa nchi hii,Mashujaa ambao hufanyiwa kumbukumbu kitaifa kila mwaka katika jamhuri yetu ya Muungano wa Tanzania.

(b) NYEUPE.

Hii maana yake ni ishara ya kwamba tunahitaji sana amani katika Jumhuri yetu ya Muungano wa Tanzania na kwamba N.R.A itasimamia kwa gharama yoyote kuweka amani nchini.Hali kadhalika hii ni ishara ya kuweka matumaini.

(c) NYEUSI.

Rangi hii ina maana ya kuashiria bara la Afrika na Waafrika.Hii ni kuonyesha kwamba shughuli na harakati za N.R.A zinafanyika katika bara la Waafrika.

III. UFAGIO NA JUA LINALOCHOMOZA.

A. JUA LINALOCHOMOZA.

Jua hili linaonekana kuchomoza asubuhi. Hii ni ishara kwamba sasa kumepambazuka au kumekucha, Jua ni ishara ya mwanga unaoondoa giza, yaani baada ya wananchi kudhulumiwa kwa namna moja au nyingine N.R.A sasa inawaletea matumaini mapya.

B. UFAGIO

Hii ni ishara kwamba kila kunapopambazuka watu huanza shughuli za kusafisha mazingira ya nyumba, ofisi zao ama sehemu zingine za kazi.

Kwa mantiki hiyo ya alama za N.R.A ni kuwa;

N.R.A kwa upande wake inayaona mabadiliko yanayohitaji kwa wananchi ni lazima kwanza wawekwe bayana ili yajulikane.

Giza lililowekwa ili mabaya yasionekane lazima liondolewe kila pahala palipojificha maovu. Kwa hali hii "JUA" ndio mwanga unaohitajika kuangaza safari yetu ya kuleta maendeleo na kujenga jamii bora.

Mwanga huo unaashiria UWAZI katika uendeshaji wa shughuli na harakati za N.R.A. Baada ya kuyaona maovu yote yaliyopo ndani ya jamii na Taifa kwa ujumla ni lazima kuyaondoa kwa kuyafagia.

Hivyo basi Alama ya "UFAGIO" ni ishara mahsusi na imesimama hapa kama nyenzo ya kuyaondoa au kuyafagia maovu hayo yanayoonekana katika Mifumo ya nchi, Sera, sheria na Taratibu mzima za uendeshaji wa shughuli za Serikali na vyombo vyake katika nchi.

